






TAARIFA ZA HARAKA KUHUSU Essential Plan

Je, nitajisajili vipi?

 nystateofhealth.ny.gov
AU

 1-855-355-5777 au
TTY: 1-800-662-1220
AU

 Kupitia usaidizi wa ana kwa ana wa bila malipo kutoka kwa msaidizi aliyeidhinishwa karibu na nyumbani au kazini kwako.

Je, mnaweza kunisaidia kwa lugha yangu binafsi?

Usaidizi unapatikana kwa lugha yako kwa simu na ana kwa ana.

Ninaweza kujiandikisha lini?

Usajili kwa Essential Plan uko wazi mwaka mzima.

NY State of Health inazingatia sheria za haki za raia za Shirikisho zinazotumika na haibagui kwa msingi wa mbari, rangi, asili ya taifa, dini, jinsi, umri, hali ya ndoa/familia, rekodi za kukamatwa, hukumu za uhalifu, utambulisho wa jinsia, mwelekeo wa kingono, sifa za kinasaba, hali ya jeshi, hali ya mhanga wa unyanyasaji wa nyumbani, na/au kulipiza kisasi.

Je, Essential Plan ni nini?

Bima ya afya kwa wakazi wa jimbo la New York. Unagharimu kiwango kidogo zaidi kuliko mipango mingine ya bima ya afya. Na unatoa manufaa sawia yaliyo msingi.

Je, ni nani anaweza kuinunua?

Watu wenye mapato madogo zaidi ambao hawahitimu kupata Medicaid au Child Health Plus.

Ukubwa wa kaya	Pato la juu zaidi unaloweza kupata
1	\$25,520
2	\$34,480
3	\$43,440
4	\$52,400

Je, inagharimu nini?

Aidha \$20 kwa mwezi kwa mtu mmoja – chini ya dola moja kwa siku au BILA CHOCHOTE.

Je, ni vipi vingine inavyo niokolea pesa ?

Haina DEDUCTIBLE (PUNGUZO), kwa hivyo mpango huu unaanza kulipia huduma yako ya afya mara moja.

Unapata HUDUMA YA UZUILIAJI BILA MALIPO kama vile chunguzi na kaguzi za daktari za mara kwa mara ili kukuweka mwenye afya.

Je, Essential Plan inashugulikia nini?

Huduma sawia zinazotolewa na bima nyingine, ikijumuisha:

- kumwona daktari, ikijumuisha madaktari bingwa
- vipimo vilivyoagizwa na daktari wako
- dawa za kuandikiwa na daktari
- huduma za wagonjwa wa kulazwa na wa kurudi nyumbani katika hospitali
- na zaidi.